

Maswali na Majibu

1. Mbona tusioe asiyemuumini?
Mungu hataki. Ina leta shida nyingi. Inatutoa kwa Mungu.
2. Nini ilifanyika Sulemani alipooa wanawake wa mataifa wengi?
Walimtoa kwa Mungu.
3. Mbona tuoe mtu anayependa Mungu?
Atatusaidia tuenende kwa njia za Mungu tukielekea kwa Ufalme.
4. Mbona tusiwe na ngono ya msaha au ngono kabla ya kuoana?
Ni kuasi Mungu. Tunaweza kukosa wokovu. Inamadhara ya kupata Ukimwi.
5. Ikiwa familia zetu zitatushurutisha kuoasi asiyemuumini, tutafanye nini?
Tusimame wima na tuweka Mungu awe wa kwanza. Tuombe usaidizi.
6. Mwenzi tunayemtafuta awe wa namna gani?
Angalia moyo. Zaidi angalia aliye wa upendo si kuangalia maumbile ya nje.
7. Tunaweza kusaidiwa namna gani ili tuwe na uwaamuzi mzuri?
Tuombe Mungu atusaidie
8. Tunaweza kuomba Mungu na tuwache atutafutie mwenzi mzuri?
Hapana. Lazima tuombe na tufanye bidii ya kutafuta mwenzetu mzuri.
9. Wakati wa kutafuta mwenzetu wa ndoa tunatakiwa tuwe na marafiki wa aina gani?
Vijana kutoka kwa eklesia na wale wanaompenda Mungu.
10. Msingi wa ndoa ya furaha ni nini katika ndoa?
Kufanya kazi pamoja kwa mapenzi na kupenda Mungu.

Mistari ya kukariri

2 Wakorintho 6:14 – 15

1 Wakorintho 13:4 – 7

Mazungumzo

Zungumza juu ya njia za ukweli ambazo zitakazo tusaidie tupate mwenzetu wa ndoa. Zungumza juu ya madhara ya kuoasi mtu asiyempenda Mungu na manufaa ya ndoa katikati ya watu waumini.

Kuandika

Andika hadithi juu ya Rebeka vile alichaguliwa kama mke wa Isaka. Tunajifunza somo gani kwa hii hadithi.

Masomo ya watoto wakubwa wa CBM



Somo la 9 Kuchagua mwenzako wa ndoa

SOMA 2 Wakorintho 6:14 – 15 na 1 Wakorintho 7:39

SOMO

Biblia inatuambia kwamba tusioe mtu asioamini au mtu aliye na imani tofauti. Ndoa na mtu asiyemuumini huwa na shida kwa utofauti wa mawazo na makusudi. Inakuwa na ugovi na kisirani. Inaweza kutoa muumini kwa imani.

Mungu ametuita sisi kwenda kwa Ufalme wake wa milele. Wajibu wetu kwa Mungu na uwe wa kwanza. Hii inahusisha hata uhusiano wetu na wenzetu wa ndoa. Inamaanisha tuchague rafiki atakayetusaidie tumpende Mungu. Kuchagua mwenzetu atakayetusaidia tuingie kwa Ufalme wa Mungu ni jambo la muhimu sana.



Biblia inatuhadharisha kuoasi mtu asiyependa Mungu au mwenye hatuna imani moja.

- ◆ Ibrahimu na Sara walihakikisha kwamba mwanao Isaka anaoa mke anayempenda Mungu (Mwanzo 24:3 – 4 na 28: 1 – 3)
- ◆ Musa aliamrisha Waisraeli wasioe watu wa mataifa waliokuwa kwa nchi hiyo (Kumbukumbu 7:3 – 4)
- ◆ Yoshua pia aliwambia Waisraeli wasioe watu wa nchi hiyo (Yoshua 23: 12 – 13)
- ◆ Wanawake wa mataifa waligeuza moyo wa Mfalme Sulemani akaacha Mungu (1 Wafalme 11:1 – 6)
- ◆ Nehemia aliambia watu ubaya wa kuoasi wale wasiojua na kumpenda Mungu (Nehemia 13:23 – 27)
- ◆ Paulo aliambia Wakorintho wasioe wasiowaumini (2 Wakorintho 6:14 – 15)

Epkana na uasherati 📖 **Soma 1 Wakorintho 6:9 – 20**

Ngono ya msaha au ngono kabla ya kuoana ni kinyume na mafundisho ya Mungu. Ngono ya msaha inamadhara ya kanuni ya uhusiano wa ndoa. Kutokea kutoaminiana katika ndoa. Na inamaanisha kutotii Mungu. Wanaofanya haya wako katika hatari ya kupoteza tumaini la wokovu na maisha mazuri kwa Ufalme wa Mungu.

Hatari nyingine ya ngono ya msaha ni UKIMWI. Hakikisha unaheba hatari hizi.

Weka amri za Mungu kwanza

Ndoa katika Bwana ni ya uzima. Tuna nafasi moja tu kupata mwenzetu mzuri wa ndoa. Tukichagua vibaya, tutakuwa na huzuni kwa maisha yetu yote. Tutavutwa na tuwe mbali na Mungu na tupoteze nafasi ya wokovu. Kuchagua mwenzetu wa ndoa ni jambo njema na uamzi wa maana sana katika maisha yetu. Tunahitajika kuomba Mungu juu yake kwa muda mrefu. Tunatakiwa Mungu atusaidie ili tufanye uamzi mwema.

Kunawezekana kuwe na ugumu na hata kushawishiwa vile kuchagua. Simama imara na weka Mungu mbele. Omba Mungu asaidie. Mambo yote yanawezekana na usaidizi kutoka kwa Mungu.

Tukiwa na msukumo wa jamii ya kuoana mtu asiye wa imani yetu, ni lazima kwanza tutii Mungu sio jamii. Katika ndoa tunakuwa na mtu tunayesaidiani kwa safari ya kuelekea kwa Ufalme wa Mungu. Hii haitawezekana tukioa asiyemuamini.


Kuchagua mwenzetu mzuri

Ni la maana kuangalia vibengele bengele fulani wakati wa kuchagua mwenzetu wa maisha. Mungu haangalii vile tunaonekana nje. Mungu huangalia moyo wa mtu. Nasi inatupasa tuangalia vivyo hivyo. Tuthaminie watu wanaopenda Mungu na wanaojaribu kumtumikia. Ni vizuri tunayemchagua awe mtu mpole, mwaminifu, wa imani na wa upendo sio wa kuvutia, mrefu, mrembo kwa sura.

Mfano wa Isaka na Rebeka 📖 **Soma Mwanzo mlango wa 24**

Tunajifunza mengi sana kutoka kwa huu mlango kuhusu kuchagua wenzetu.

- ◆ Waumini wasioe wasio waumini. *mstari wa 3*
- ◆ Tuwe na juhudi ya kutafuta mwenzi mwema – Eliezari alitumwa kwa safari ndefu ili kutafuta Rebeka. *mstari wa 4*
- ◆ Tuamini Mungu na tumwombe atusaidie. *mstari wa 7*
- ◆ Tuwe na busara tukitafuta mwenzi aliye mwema, mkarimu na anayependa Mungu – Eliezari hakuomba mwanamke wa sura nzuri, lakini aliomba awe mwema na mkarimu, awape ngamia maji. *mstari wa 14*
- ◆ Ibrahimu na Eliezari waliamini Mungu na wakataka uongozi wake. Tunatakiwa tufanye vivyo hivyo. *mstari wa 12*
- ◆ Ikiwezekana tujitahidi kutafuta mwenzi mzuri. Tusiwachie Mungu pekee. *mstari wa 10*



Tunawezaje kupata mwenzi anayependa Mungu?

Ni la muhimu kuwa na marafiki wanaopenda Mungu. Kuwa na urafiki na vijana wa eklesia yako. Mue mkikutana nao. Panga michezo pamoja. Kuwa na shughuli pamoja kama kufundisha wengine au kazi fulani fulani. Soma Biblia pamoja. Himizani kukuwa na mwenendo wa utawa.

Upendo wa kweli kwa ndoa 📖 **Soma 1 Wakorintho 13**

Katika ndoa ya Kikristo tujitahidi iwezekanavyo kuwa na upendo kwa vitendo. Tuwe pamoja kwa kila jambo tukisaidiana kuonyesha upendo kwa Mungu. Huu ndio msingi wa ndoa ya furaha katika Bwana.

Mume na mke waonyeshe upendo na kila mmoja ajali mwenzake kwa njia zote. Upendo wa Yesu ni msingi wa wema na kutufunganisha pamoja kama mume na mke. Ni baraka kuu ndoa zetu zikijengwa kwa kupendana na upendo wa Mungu. Tena ni mfano mzuri kwa watoto wetu.